**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA



# TAARIFA YA DAWA ZA KULEVYA





2019-2020

SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS

**TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR**

# TAARIFA YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2019 - 2020

**MAELEZO YA MWENYEKITI WA TUME**

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya afya njema na hali ya usalama nchini. Pia napenda kuchukua fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu atupe na sisi rehema na baraka zake katika maisha yetu yote na nchi yetu kuendelea kuwa na amani na utulivu AMIN.

Serikali kwa kushirikiana na washirika wa ndani na nje ya nchi imefanya jitihada za kukabiliana na madhara na matumizi ya Dawa za Kulevya pamoja na kudhibiti uingizaji na usambazaji wa dawa hizo.

Athari zitokanazo na matumizi ya Dawa za Kulevya zimeendelea kuathiri sekta za uzalishaji na hivyo kudhoofisha ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Matumizi hayo yamekuwa yakiathiri afya za Wazanzibari hasa vijana ambao ni nguvu kazi ya taifa letu.

Maendeleo ya Taifa letu hutegemea zaidi nguvu kazi ya vijana wenye muelekeo makini na hivyo hatma ya nchi yetu ya kufikia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (Sustainable Development Goals) pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi 2020 -2025 kamwe hayataweza kufikiwa iwapo vijana wataendelea kujitumbukiza katika janga la matumizi ya mihadarati.

Hali halisi ya kesi zinazohusiana na Dawa za Kulevya zinakabiliana na changamoto nyingi ambazo moja wapo ni jamii pamoja na wasimamizi wa sheria katika maeneo tofauti ya mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya kutotimiza wajibu wao.

Uadilifu na uwajibikaji ni rasilimali muhimu sana katika kusimamia vita dhidi ya Dawa za Kulevya nchini. Hivyo, kwa nafasi zetu na kupitia taasisi zetu inatupasa kila mmoja wetu kujidhatiti na kutimiza wajibu wake ipasavyo katika kufanikisha vita hii.

Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza washirika wote kwa kutoa ushirikiano katika kukabiliana na tatizo la Dawa za kulevya nchini. Tatizo hili ni mtambuka hivyo linahitaji ushirikiano mkubwa na washirika mbali mbali wa sekta tofauti. Vile vile, naiomba jamii kushiriki kwa dhati kabisa katika kukabiliana na tatizo hili la matumizi na usafirishaji wa Dawa za Kulevya kwa kutoa taarifa za wahalifu kwa vyombo vinavyohusika na udhibiti wa dawa za kulevya.

**Hemed Suleiman Abdulla**
**Mwenyekiti**
**Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya**
**Zanzibar.**

## DIBAJI

Taarifa ya hali ya Dawa za Kulevya nchini imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Nam.8 cha Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nam.9 ya mwaka 2009. Lengo la taarifa hii ni kuonesha hali halisi ya Dawa za Kulevya ilivyokuwa kwa mwaka 2019 -2020.

Taarifa hii itasaidia kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu tatizo la Dawa za Kulevya na kuonesha changamoto zilizopo ili wahusika mbalimbali wakiwemo wananchi, waweze kushiriki na kuimarisha mapambano dhidi ya matumizi na usafirishaji wa Dawa za Kulevya.

Taarifa hii imeandaliwa kwa kutumia takwimu zilizokusanywa kutokana na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Tume pamoja na taarifa kutoka kwa washirika wa udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini. Vile vile, taarifa hii imejumuisha takwimu kutoka Shirika la Kimataifa la kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC).

Taarifa hii imegawika katika sehemu kuu sita. Sehemu ya kwanza inaelezea historia ya Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na historia ya Sheria ya Dawa za Kulevya. Sehemu ya pili inaelezea tatizo la Dawa za Kulevya kwa kuonesha madhara na hali ya usafirishaji na matumizi ya Dawa za Kulevya katika miaka ya 2012- 2020. Sehemu ya tatu inaelezea juhudi za Serikali katika kudhibiti usafirishaji wa Dawa za Kulevya kwa mwaka 2019 -2020. Sehemu ya nne inaelezea juhudi za Serikali katika kudhibiti matumizi ya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2019-2020. Sehemu ya tano inaelezea hali ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika kudhibiti Dawa za Kulevya kwa kipindi cha 2019-2020 na sehemu ya sita inaeleza mafanikio, changamoto na hatua za baadae.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru watendaji na wadau wote waliowasilisha taarifa kutoka sehemu zao husika ambazo kwa kiasi kikubwa zimesaidia kufanikisha uandaaji wa taarifa hii itakayoleta mafanikio kwa taasisi pamoja na Taifa kwa ujumla.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum**
**Waziri wa Nchi,**
**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais,**
**Zanzibar**

# YALIYOMO


**MAELEZO YA MWENYEKITI WA TUME ........ i**

**DIBAJI ........ ii**

**YALIYOMO ........ iii**

**ORODHA YA VIELELEZO NA JADUWELI ........ vi**

**VIFUPISHO ........ vii**

**SEHEMU YA KWANZA: ........ 1**

**TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA ........ 1**

**1.1 UTANGULIZI ........ 1**

1.2 MWENENDO WA SHERIA ZA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA ........ 1

1.3 HISTORIA YA TUME ........ 2

**SEHEMU YA PILI: ........ 3**

**TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR ........ 3**

2.1 MADHARA YA DAWA ZA KULEVYA ........ 3

2.1.1 Kiafya ........ 3

2.1.2 Kijamii ........ 3

2.1.3 Kiuchumi ........ 3

2.1.4 Kimazingira ........ 3

2.1.5 Kisiasa ........ 4

2.2 USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA DAWA ZA KULEVYA ........ 4

2.2.1 Mwenendo wa idadi ya kesi za Dawa za Kulevya. ........ 4

***Kielelezo Nam.1: Mwenendo wa Kesi za Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2012-2020 ........ 4***

2.2.2 Mwenendo wa Viwango vya Dawa za kulevya ........ 5

***Kielelezo Nam.2: Mwenendo wa viwango (kg) vya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2012-2020 ........ 5***

***Jaduweli namba. 2 mwenendo wa uendeshaji wa kesi mwaka Juni 2019 - 2020 ........ 7***

2.2.3 Usambazaji wa Bangi na Heroini ........ 7

***Kielelezo Nam.3 kiwango cha Bangi (kg) kilichokamatwa mwaka 2012-2020 ........ 8***

***Kielelezo Nam. 4. Kiwango cha Heroini (kg) kilichokamatwa mwaka 2012-2020 ........ 8***

2.3 MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA ........ 9

2.3.1 Kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya duniani ........ 9

2.3.2 Kiwango cha matumizi ya Dawa za Kulevya Zanzibar ........ 9

2.3.3 Sababu zinazopelekea matumizi ya Dawa za kulevya ........ 9

2.3.4 Tiba na marekebisho ya tabia ........ 9

***Jaduweli Nam 3. Idadi ya watu 9379 waliopata huduma ya upataji nafuu mwaka 2019-2020 ........ 10***

**SEHEMU YA TATU:** ........................................................................ **11**

**JUHUDI ZA SERIKALI KATIKA UDHIBITI USAMBAZAJI WA DAWA ZA KULEVYA MWAKA 2019-2020** ........................................................................ **11**

3.1 UKAMATAJI WA DAWA ZA KULEVYA ........................................ 11

3.1.1 Kiwango cha Dawa za Kulevya Kilichokamatwa ........................................ 11

***Jaduweli Nam.4 Kiwango kulingana na Aina ya Dawa ya Kulevya mwaka 2019-2020*** ........... **11**

3.1.2 Kesi za Dawa za Kulevya zilizoripotiwa ........................................ 11

***Jaduweli Nam 7: Idadi ya kesi kulingana na Sehemu iliyoripoti kesi hizo mwaka 2019-2020*** .. **12**

3.1.3 Mchanganuo wa Viwango vya dawa kimaeneo ya ukamataji ........................................ 13

***Kielelezo namba.5 kiwango cha heroin kilichokamatwa 2019-2020*** ........................................ **13**

***Kielelezo namba.6 kiwango cha Bangi kilichokamatwa 2019-2020*** ........................................ **13**

**Kielelezo namba.7 kiwango cha mirungi kilichokamatwa 2019-2020** ........................................ **14**

***Kielelezo namba.8 kiwango cha valiam kilichokamatwa 2019-2020*** ........................................ **14**

***Kielelezo namba.9 kiwango cha Kokeni kilichokamatwa 2019-2020*** ........................................ **14**

3.2 MALI ZILIZOHUSIKA NA UHALIFU WA DAWA ZA KULEVYA ........................................ 15

3.3 MAFUNZO, MIKUTANO NA VIKAO. ........................................ 15

3.2.1 Mikutano ya Wasimamizi wa Sheria ........................................ 15

3.2.2 Mafunzo kwa Wahusika wa Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya ........................................ 16

3.2.3 Vikao vya Tume na vya Kamati ya Kitaalamu ........................................ 16

3.2.4 Mikutano ya Uchunguzi na Operesheni ........................................ 16

**SEHEMU YA NNE** ........................................................................ **17**

**JUHUDI ZA SERIKALI KATIKA KUPUNGUZA MATUMIZI NA MADHARA YA DAWA ZA KULEVYA** ........................................................................ **17**

4.1 ELIMU JUU YA ATHARI YA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA ........................................ 17

4.1.1 Kuyafikia makundi mbalimbali ........................................ 17

***Jaduweli Nam.9: Idadi ya waliopatiwa elimu juu ya athari ya matumizi ya Dawa za Kulevya mwaka 2019 - 2020*** ........................................ **17**

4.1.2 Kutoa vipeperushi ........................................ 17

4.1.3 Kurusha vipindi vya Redio na Televisheni ........................................ 17

4.2 KINGA YA MSINGI DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA ........................................ 18

***Jaduweli Nam.10: Idadi ya waliopatiwa elimu juu ya athari ya Dawa za Kulevya kupitia program ya*** ........................................ **18**

***kinga ya msingi mwaka 2019-2020*** ........................................ **18**

4.3 KUZIWEZESHA PROGRAMU ZA UPATAJI NAFUU. ........................................ 18

4.3.1 Kusaidia nyumba za upataji nafuu (Sober Houses) ........................................ 18

***Jaduweli Nam.11 Idadi ya watu waliojiunga na huduma ya upataji nafuu kwa mwaka 2019-2020*** **...... 19**
4.3.2 Mikutano ya Tiba ya Kifamilia ...... 19
4.3.3 Kuwajengea uwezo watumiaji baada ya kupata nafuu ...... 19
4.3.4 Kupunguza Madhara ya kiafya kwa watumiaji wa Dawa za Kulevya ...... 19
4.4 KUENDESHA MIKUTANO YA WADAU ...... 20
4.5 KITUO CHA TIBA NA MAREKEBISHO YA TABIA - KIDIMNI ...... 20
**SEHEMU YA TANO ...... 21**
**USHIRIKIANO WA NDANI YA NCHI NA WA KIMATAIFA ...... 21**
5.1 USHIRIKIANO NA TAASISI ZA NDANI YA NCHI ...... 21
5.2 USHIRIKIANO WA KIMATAIFA ...... 22
5.2.1 SHIRIKA LA KIMATAIFA LA KUZUIA UHALIFU NA DAWA ZA KULEVYA (UNODC) ...... 22
5.2.2 DRUG ENFORCEMENT ADMINISTRATION (DEA) ...... 22
5.2.3 UNITED KINGDOM (UKaids) & UK BORDER FORCE ...... 23
5.2.4 US DEPARTMENT OF DEFENCE ...... 23
**SEHEMU YA SITA ...... 24**
**MAFANIKIO, CHANGAMOTO, HATUA ZA BAADAE NA HITIMISHO ...... 24**
6.1 MAFANIKIO ...... 24
6.2 CHANGAMOTO ...... 25
6.3 HATUA ZA BAADAE ...... 25
6.4 HITIMISHO ...... 26

**ORODHA YA VIELELEZO NA JADUWELI**

*Kielelezo Nam.1: Mwenendo wa Kesi za Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2012-2020*........................**4**

*Kielelezo Nam.2: Mwenendo wa viwango (kg) vya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2012-2020* .......**5**

*Jaduweli namba. 2 mwenendo wa uendeshaji wa kesi mwaka Juni 2019 - 2020* .............................**7**

*Kielelezo Nam.3 kiwango cha Bangi (kg) kilichokamatwa mwaka 2012-2020* ................................**8**

*Kielelezo Nam. 4. Kiwango cha Heroini (kg) kilichokamatwa mwaka 2012-2020* ..........................**8**

*Jaduweli Nam 3. Idadi ya watu 9379 waliopata huduma ya upataji nafuu mwaka 2019-2020* .....**10**

*Jaduweli Nam.4 Kiwango kulingana na Aina ya Dawa ya Kulevya mwaka 2019-2020* ...............**11**

*Jaduweli Nam 7: Idadi ya kesi kulingana na Sehemu iliyoripoti kesi hizo mwaka 2019-2020* ......**12**

*Kielelezo namba.5 kiwango cha heroin kilichokamatwa 2019-2020*.............................................**13**

*Kielelezo namba.6 kiwango cha Bangi kilichokamatwa 2019-2020*..............................................**13**

Kielelezo namba.7 kiwango cha mirungi kilichokamatwa 2019-2020 ...........................................**14**

*Kielelezo namba.8 kiwango cha valiam kilichokamatwa 2019-2020* .............................................**14**

*Kielelezo namba.9 kiwango cha Kokeni kilichokamatwa 2019-2020*.............................................**14**

*Jaduweli Nam.9: Idadi ya waliopatiwa elimu juu ya athari ya matumizi ya Dawa za Kulevya mwaka 2019 - 2020* ...................................................................................................................**17**

*Jaduweli Nam.10: Idadi ya waliopatiwa elimu juu ya athari ya Dawa za Kulevya kupitia program ya kinga ya msingi mwaka 2019-2020* ...........................................................................**18**

*Jaduweli Nam.11 Idadi ya watu waliojiunga na huduma ya upataji nafuu kwa mwaka 2019-2020*..........................................................................................................................**19**

**VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| DEA | Drug Enforcement Administration |
| DPP | Director of Public Prosecutions |
| FIU | Financial Intelligence Unity |
| KG | Kilogramme |
| KMKM | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo |
| MAT | Medically Assisted Therapy |
| RCZ | Recovery Community Zanzibar |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SUZA | State University of Zanzibar |
| TB | Tuberculosis |
| TKKUDK | Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UMATI | Uzazi na Malezi Bora Tanzania |
| UNODC | United Nations Office on Drugs and Crime |
| VVU | Virusi Vya UKIMWI |
| ZAECA | Zanzibar Anti-corruption and Economic Crimes Authority |
| ZANPUD | Zanzibar People Who Used Drugs |
| ZAYADESA | Zanzibar Youth Education Development Support Association |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Cooperation |
| ZIHTLP | Zanzibar Intergrated HIV, TB, and Leprocy |
| ZYF | Zanzibar Youth Forum |

# SEHEMU YA KWANZA:
# TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

## 1.1 UTANGULIZI

Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar, imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nam. 9 ya mwaka 2009. Taasisi hii inaongozwa na Mwenyekiti ambae huteuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (2) (a) cha Sheria hiyo. Wajumbe kutoka taasisi mbali mbali–wakiwemo Mawaziri, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Watendaji kutoka taasisi zinazohusika na mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya na Mkurugenzi Mtendaji anakuwa Katibu wa Tume.

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku, Tume inafanya kazi kupitia Sekretarieti inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji ambae ndie Afisa Mtendaji Mkuu wa Tume na mwenye dhamana ya utendaji wa kazi hizo.

Kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Nam. 9 ya Mwaka 2009, kifungu cha 8, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya inatakiwa kuandaa na kutoa Taarifa ya mwaka ya Hali halisi ya Dawa za Kulevya Nchini na baadae iwasilishwe Baraza la Wawakilishi. Madhumuni ya taarifa hii ni kuelezea tatizo la Dawa za Kulevya lilivyokuwa kwa mwaka husika kwa kuainisha hali halisi ya tatizo, mafanikio yaliyofikiwa katika kukabiliana na tatizo hilo pamoja na hatua zinazopaswa kuimarishwa ili kudhibiti tatizo hilo.

## 1.2 MWENENDO WA SHERIA ZA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Sheria ya mwanzo ya Dawa za Kulevya ilitungwa mwaka 1915, ambayo iliyojulikana kama ”*The abuse of Opiates Decree No. 5 of 1915”*. Sheria hii ilifutwa na Sheria Nam.11 ya mwaka 1927 iliyoitwa Sheria ya Dawa Hatari za Kulevya (*The Dangerous Drugs Decree No.11 of 1927*) ambayo baadae ilikuja kuwa *Sura ya 76* ya Sheria za Zanzibar kupitia marekebisho ya mwaka 1959. *Sura ya 76* iliendelea kutumika hata baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 hadi 1986 ilipofutwa na Sheria ya Ufamasia na Dawa Hatari za Kulevya (*The Pharmaceuticals and Dangerous Drugs Act No.6 of 1986*). Sheria hii Nam.6 ya 1986 nayo ilifutwa na Sheria Nam.16 ya 2003 iliyojulikana kama Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya (*The Drugs & Prevention of Illicit Traffick Drugs Act No.16 of 2003*). Sheria Nam.16, nayo

ilikuja kufutwa rasmi na Sheria Nam.9 ya 2009 ambayo ndiyo inayotumika mpaka sasa na imekuwa ikifanyiwa marekebisho kila mara kwa mujibu wa mahitaji.

### 1.3 HISTORIA YA TUME

Katika kuimarisha jitihada za kupambana na Dawa za Kulevya, mwaka 1996 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha taasisi maalumu ya kupambana na Dawa za Kulevya iliyojulikana kwa jina la Idara ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya chini ya Ofisi ya Waziri Kiongozi. Mwaka 2000 taasisi hii ilihamishiwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mwaka 2003 ilitungwa Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Nam. 16 ya Mwaka 2003 ambayo ilipelekea Idara hiyo kubadilishwa jina na kuitwa Idara ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Kurekebisha Tabia. Sheria hii Nam. 9 ya 2009 ilifuta Sheria Nam. 16 ya 2003 na ndio iliyoanzisha Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar ambayo inafanya kazi hadi leo.

# SEHEMU YA PILI:
# TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR

## 2.1 MADHARA YA DAWA ZA KULEVYA

Madhara yatokanayo na Dawa za Kulevya yanaathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya nchi katika maeneo mbali mbali. Matumizi, usafirishaji na usambazaji wa dawa hizo umepelekea matokeo mabaya ya kiafya, ustawi wa jamii, uchumi na mazingira.

### 2.1.1 Kiafya

Watumiaji wa Dawa za Kulevya wapo katika hatari ya kupata maradhi mbalimbali yakiwemo ugonjwa wa mapafu, akili, moyo, utegemezi wa Dawa za Kulevya, shindikizo la damu, na maambukizi ya VVU/UKIMWI na homa ya Ini B na C. Aidha, matumizi ya Dawa za Kulevya kwa kiwango kikubwa (overdose) husababisha vifo vya ghafla hasa miongoni mwa wanaojidunga sindano.

### 2.1.2 Kijamii

Matumizi ya Dawa za Kulevya yanahusishwa na mfarakano wa kifamilia hasa ikiwa mmoja wao ni mtumiaji, kutengwa na jamii, mmong'onyoko wa maadili na kuongezeka kwa watoto wanaozurura mitaani. Aidha, usalama wa jamii pia umekuwa hatarini kwa kuwa watumiaji wengi wanajihusisha na vitendo vya uhalifu kama vile wizi, magenge ya uporaji, ubakaji na uharibifu wa mali na miundombinu.

### 2.1.3 Kiuchumi

Matumizi ya Dawa za Kulevya yanasababisha uzalishaji mdogo unaotokana na kupungua nguvu kazi ya Taifa, ukosefu wa ajira, maradhi na vifo vya mapema. Vile vile, hupunguza pato la Taifa na familia ambalo linatumika zaidi kuwahudumia na kuwatibu watumiaji hao. Aidha, usafirishaji wa Dawa za Kulevya huathiri ukuaji wa uchumi na kusababisha kuwepo kwa utakatishaji wa fedha haramu, mfumko wa bei na ongezeko la rushwa.

### 2.1.4 Kimazingira

Shughuli zinazohusiana na Dawa za Kulevya kama vile ulimaji na uzalishaji katika maabara zisizokuwa rasmi zinachangia ongezeko la uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Kilimo cha Dawa za Kulevya kinahusisha matendo ya uvunjaji wa Sheria ambapo kinajumuisha, ukataji na uondoshaji wa miti kwa lengo la kupata eneo kubwa la kilimo. Utupaji ovyo bomba na sindano kwenye maeneo ya wazi husababisha majanga kwa wapita njia na watoto wanaocheza katika

maeneo hayo. Vifaa hivyo vinavyotupwa ovyo vinaweza kuongeza ajali na kusambaza magonjwa yanayoambukiza kwa njia ya damu kama UKIMWI na Homa ya Ini.

### 2.1.5 Kisiasa

Kutokana na uwezo wao mkubwa wa kifedha wauzaji wa Dawa za Kulevya wanaweza kujiingiza katika shughuli za kisiasa hivyo kuwepo uwezekano wa kupata viongozi wanaojihusisha na Dawa za Kulevya. Vile vile wauzaji hao wanaweza kufadhili chaguzi na kuwaweka watu wao madarakani ili kulinda maslahi yao. Hali hii inaweza kuathiri mustakabali wa nchi na kuongeza ugumu katika mapambano hayo.


## 2.2 USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA DAWA ZA KULEVYA

Maumbile ya visiwa kijografia bado yanaleta ugumu katika kudhibiti uingiaji wa Dawa za Kulevya Zanzibar. Kwa mujibu wa taarifa kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC) nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini zinatajwa kuwa ni miongoni mwa njia za kupitishia dawa za kulevya aina ya heroini zinazotoka Afghanistani na kuelekea Asia, Mashariki ya Kati, Ulaya na Marekani.

Kupitia Ripoti za Kitengo cha Polisi cha Kupambana na Dawa za Kulevya zimeonesha katika kipindi cha miaka 9 iliyopita (2012-2020) jumla ya watuhumiwa 3,810 wakiwemo wanaume 3,577 na wanawake 233 wamekamatwa nchini wakijihusisha na uhalifu wa Dawa za kulevya. Katika kipindi hicho hicho jumla ya kilo 51.5 za heroini, kilo 2,946 za bangi, kilo 5.4 za valiamu na kilo 19.71 za kokeni zilikamatwa.

### 2.2.1 Mwenendo wa idadi ya kesi za Dawa za Kulevya.

*Kielelezo Nam.1**:** Mwenendo wa Kesi za Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2012-2020*





***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***

Kielelezo nam.1 kinaonesha kuwa idadi ya kesi za Dawa za Kulevya ilikuwa chini kabla ya mwaka 2016. Aidha idadi hiyo imeongezeka kuanzia mwka 2016 hadi mwaka 2018 na kushuka kidogo mwaka 2019-2020.

### 2.2.2 Mwenendo wa Viwango vya Dawa za kulevya

*Kielelezo Nam.2: Mwenendo wa viwango (kg) vya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2012-2020*




***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***

Mwenendo wa Viwango vya dawa za kulevya vinavyokamatwa vinaonekana kwenda sambasamba na mwenendo wa idadi ya kesi kwakuwa viwango hivyo vinaonekana kuanza kupanda mwishoni mwa 2016 hadi mwaka 2018 na 2019 na kushuka katika mwaka 2020.

Uchambuzi wa taarifa mbali mbali zinazowasilishwa na Mamlaka zinazoshughulikia kesi hizo unaashiria kuwa asilimia kubwa ya mabadiliko ya idadi pamoja na kiwango cha dawa za kulevya yanayoonekana katika kielelezo Namba 1 na Namba 2 yanasababishwa na mabadiliko ya hatua za usimamizi wa sheria, mbinu za ukamataji pamoja na mbinu za usambazaji.

Kabla ya mwaka 2016 idadi ya kesi zilizokamatwa ilikuwa ipo chini wakati uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya ulikuwa ukifanyika wazi wazi katika maeneo mengi. Hii inamaanisha kwamba kasi na mbinu za ukamataji hazikuwa zenye kuridhisha. Kuanzia mwaka 2016 baada ya sheria kufanyiwa marekebisho kadhaa na kuongezeka kwa kasi ya mapambano watuhumiwa wengi walikamatwa na kusababisha idadi ya kesi hizo kuongezeka kwa miaka 3 mfululizo hadi kufikia asilimia 73.6 ya ongezeko la idadi ya kesi (kutoka kesi 183 mwaka 2016 hadi kesi 694 mwaka 2018).

Aidha ripoti zinaonesha kuwa ingawaje kasi ya ukamataji wa dawa za kulevya iliongezeka kuanzia mwaka 2016 usambazaji wa dawa hizo haukupungua kwa sababu hakukuwa na usimamizi mzuri wa sheria jambo lilipolekea kesi nyingi kufungwa katika vituo vya polisi na zile zilizofika Mahkamani zilifutwa ama kufungwa na watuhumiwa kurudi mitaani na kuendelea na uhalifu bila ya hofu. Kwa mfano kati ya kesi zote zilizokamatwa mwaka 2016, kesi 106 (30%) zilifungwa polisi na kesi 92 (26%) zilifungwa Mahkamani. Mwaka 2017 wastani wa 50% zilikwama katika upelelezi, 13% zilifungwa polisi na 4% zilifungwa mahkamani. Mwaka 2018 kati ya kesi zote 30% ya kesi hizo zilibakia katika upelelezi, 10% zilifungwa polisi na 2% zilifungwa Mahkamani - jaduweli nam 2**.**

*Jaduweli namba1 Mwenendo wa uendeshaji wa kesi mwaka 2016 -2018*

| HATUA YA KESI | ZINAENDELEA MAHKAMANI | ZIMEFUNGWA MAHKAMANI | ZIMEFUNGWA POLISI | ZIMEPATA HATIA | MKEMIA | ZIPO KWA DPP | U/I | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | | | | | | | | |
| IDADI YA KESI | 84 | 92 | 106 | 19 | | 6 | 47 | 354 |
| ASILIMIA | 24% | 26% | 30% | 5% | | 2% | 13% | |
| 2017 | | | | | | | | |
| IDADI YA KESI | 166 | 29 | 89 | 23 | 18 | 19 | 350 | 694 |
| ASILIMIA | 24% | 4% | 13% | 3% | 3% | 3% | 50% | |
| 2018 | | | | | | | | |
| IDADI YA KESI | 180 | 14 | 64 | 19 | 7 | 57 | 117 | 654 |
| ASILIMIA | 28% | 2% | 10% | 3% | 1% | 9% | 18% | |

***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2019***

Mwaka 2019 - 2020: Sababu iliyopelekea kupungua kwa idadi ya kesi zilizokuwa zikifungwa vituoni na kuongeza idadi ya kesi zilizopata hati ya mashtaka ni kutokana na maafisa wa upelelezi kujengewa uwezo na mbinu mpya za kupambana na uhalifu huo. (Jaduweli namba 2)

*Jaduweli namba. 2 mwenendo wa uendeshaji wa kesi mwaka Juni 2019 - 2020*

| HATUA YA KESI | Zipo Mahakamani | Zimepata Hatia | zimeachiwa huru | Zimefungwa Polisi | Zipo kwa DPP | Zimepata Hati ya Mashtaka | Chini ya Upelelezi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **IDADI** | 281 | 28 | 5 | 30 | 13 | 183 | 140 |
| **ASILIMIA** | 41% | 4% | 1% | 4% | 2% | 27% | 21% |

***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***


### 2.2.3 Usambazaji wa Bangi na Heroini

Bangi na Heroini ni aina ya dawa za kulevya ambazo husambazwa na kutumika kwa kiwango kikubwa zaidi Zanzibar ukilinganisha na aina nyengine ya dawa za kulevya. Hii inatokana na upatikanaji mkubwa wa dawa hizi kutoka maeneo mbali mbali. Heroini inayopatikana Zanzibar ni ile inayotoka nchi za Mashariki ya mbali na kwenda Ulaya na Asia kupitia Zanzibar. Bangi inayopatikana Zanzibar mara nyingi hutokea katika maeneo mbali mbali ya Tanzania Bara. Kulingana na taarifa za ukamataji zilizoripotiwa na Mamlaka mbali mbali kutoka 2012 hadi 2020, jumla ya *kilogramu 2064.006* za dawa za kulevya zilikamatwa ambapo kilogramu 1868.382 sawa na 90.52% zilikuwa ni bangi ikafuatiwa na Heroini kilogramu 51.518 sawa na 2.5% na kilogramu 144.106 (6.98%) ilijumuisha aina nyengine za dawa za kulevya ikiwemo Kokeni, Valiam na Mirungi.

**Mwenendo wa kiwango cha Bangi**

Katika kipindi cha 2012 – 2020 kiwango kikubwa cha bangi kiliripotiwa kukamatwa katika mwaka 2018 ukafuatiwa na mwaka 2019 wakati kiwango kidogo kikiripotiwa katika mwaka 2016. Kwa mwaka 2020 kiwango cha bangi kilichokamatwa kimeshuka kwa asilimia kubwa (94.36%) kikilinganishwa na kiwango hicho mwaka 2019.

*Kielelezo Nam.3 kiwango cha Bangi (kg) kilichokamatwa mwaka 2012-2020*





***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***

**Mwenendo wa viwango vya Heroini**

Kiwango kikubwa cha heroini kilichokamatwa kwa mwaka 2012-2020 kinaonekana kuripotiwa katika mwaka 2014 (kilogramu 12.961) ukifuatiwa na mwaka 2020 (kilogramu 9.297) wakati kiwango kidogo cha heroini kimeripotiwa kukamatwa katika mwaka 2015 (kilogramu1.629). Aidha , kiwango hicho kimepanda kwa asilimia 3.2 kutoka 2019 hadi 2020 (kutoka kilogramu 6.046 mwaka 2019 hadi kilogramu 9.297 mwaka 2020).

*Kielelezo Nam. 4. Kiwango cha Heroini (kg) kilichokamatwa mwaka 2012-2020*




***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***

## 2.3 MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

### 2.3.1 Kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya duniani

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC - 2020) inakadiriwa kuwa zaidi ya watu robo bilioni (milioni 271/5.5%) wenye umri wa miaka 15-64 duniani kote wanatumia Dawa za Kulevya. Kati ya hao, watu Milioni 35 (13%) wanakabiliwa na tatizo la utegemezi na watu milioni 11.3 (0.23%) wanatumia dawa kwa njia ya kujidunga sindano.

### 2.3.2 Kiwango cha matumizi ya Dawa za Kulevya Zanzibar

Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2010 uliofanywa na UNODC, inakadiriwa kuwa watu 7,000 mpaka 10,000 wanatumia Dawa za Kulevya Zanzibar, na kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Kitengo Shirikishi cha Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma (ZIHTLP - 2019) watu 2,200 wanatumia dawa za kulevya kwa njia za kujidunga sindano. Dawa inayotumiwa zaidi ni bangi na inayotumika kujidunga ni heroini kwa wanawake na wanaume lakini tabia hii imeshamiri zaidi kwa vijana wa kiume.

### 2.3.3 Sababu zinazopelekea matumizi ya Dawa za kulevya

Matatizo ya Dawa za Kulevya Zanzibar yanachochewa na sababu mbali mbali zikiwemo shindikizo rika, kuiga, malezi mabaya, binaadamu kutokuwa na uwezo wa kujikwamua na matatizo anayokabiliana nayo, kuwa na marafiki wenye tabia mbaya.

Sababu nyengine za msingi zinazoshawishi utumiaji wa dawa za kulevya ni kutokuwa na shughuli za kufanya na kutokutambua athari ya Dawa za Kulevya. Aidha, shindikizo la maendeleo ya kiuchumi, kisayansi na teknolojia, upatikanaji wa Dawa za Kulevya na maendeleo ya utalii ni miongoni mwa sababu hatarishi zinazowafanya vijana wa Zanzibar watumbukie katika matumizi ya Dawa za kulevya.

### 2.3.4 Tiba na marekebisho ya tabia

Jitihada kubwa zimefanywa ili kuhakikisha upatikanaji wa matibabu ya Dawa za Kulevya na huduma za marekebisho ya tabia zenye lengo la kuwatoa watu katika utegemezi wa dawa za kulevya na kuwarudisha katika hali ya kawaida. Njia tofauti za matibabu zinatolewa nchini zikiwemo ushauri nasaha kuhusiana na dawa za kulevya, kutolewa sumu mwilini, tiba za mabadiliko ya tabia na kujitambua, matibabu ya dharura, kuhamasishana na kusaidiana katika makundi rika.

Mfumo wa huduma ya upataji nafuu unaoendeshwa katika nyumba maalum maarufu kama “Sober house” umeanzishwa hapa Zanzibar mwaka 2009 ambao hujikita zaidi na matibabu ya muongozo wa hatua 12. Taarifa za mafanikio ya mfumo huo kwa kipindi cha miaka 12 inaonekana katika *Jaduweli Nam. 5*

*Jaduweli Nam 3. Idadi ya watu 9379 waliopata huduma ya upataji nafuu mwaka 2019-2020*

| | IDADI | ASILIMIA |
|---|---|---|
| **Waliofanikiwa kuachana na matumizi ya dawa za kulevya** | **3271** | 35% |
| **Waliorejea matumizi ya dawa za kulevya** | **4975** | 53% |
| **Wamebadilisha utumiaji (kutoka heroini kwenda dawa nyengine)** | **284** | 3% |
| **Hakuna taarifa zao (wamesafiri nje ya nchi)** | **849** | 9% |

***Chanzo: TKKUDK, 2021***

# SEHEMU YA TATU:
# JUHUDI ZA SERIKALI KATIKA UDHIBITI USAMBAZAJI WA DAWA ZA KULEVYA MWAKA 2019-2020

## 3.1 UKAMATAJI WA DAWA ZA KULEVYA

Serikali katika kupambana na uhalifu wa Dawa za kulevya ni kuwezesha shughuli za ukamataji wa wahalifu wa dawa za kulevya pamoja na uendeshaji wa kesi za Dawa za Kulevya nchini.

### 3.1.1 Kiwango cha Dawa za Kulevya Kilichokamatwa

Kutokana na juhudi mbalimbali za Serikali katika kudhibiti usambazaji na usafirishaji wa Dawa za Kulevya kwa mwaka 2019 -2020, Jumla ya kilogramu 783 za Dawa za Kulevya aina mbalimbali zilikamatwa katika maeneo tofauti ya Zanzibar kama inavyoonekana katika jadweli lilnalofuata:

*Jaduweli Nam.4 Kiwango kulingana na Aina ya Dawa ya Kulevya mwaka 2019-2020*

| AINA YA DAWA YA KULEVYA | UZITO (Kg) | | JUMLA |
|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | |
| **Heroini** | 6.26 | 9.287 | 15.5 (2%) |
| **Bangi** | 684.36 | 38.043 | 722.4 (92.3%) |
| **Mirungi** | 9.15 | 33.647 | 42.8 (5.5%) |
| **Valiam** | 0.01 | 1.22 | 1.23 (0.2%) |
| **Kokeni** | 0.96 | 0.02 | 0.98 (0.1%) |
| **JUMLA** | 701 | 82.23 | 783.0 |

***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***

### 3.1.2 Kesi za Dawa za Kulevya zilizoripotiwa

Ukamataji ni moja kati ya jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika udhibiti wa Dawa za Kulevya. Katika kipindi cha miaka miwili 2019-2020 kumeripotiwa jumla ya kesi **957** (503 mwaka 2019 na 454 mwaka 2020) katika vituo vya Polisi vya Mikoa yote ya Zanzibar pamoja na Kitengo Maalumu cha Polisi cha Kupambana na Dawa za Kulevya (ADU). Kesi hizo zina jumla ya watuhumiwa **526** ambapo watuhumiwa **514** ni wanaume na **12** ni wanawake (*takriban ni sawa na wastani wa mtuhumiwa 1 kwa kila kesi*). Mkoa wa Mjini Magharibi ndio Mkoa ulioripoti kesi nyingi **291** (30%), ADU iliripoti kesi **201** (21%), Mkoa wa Kusini Unguja kesi **173** (18%), Mkoa wa Kaskazini Unguja ulioripoti kesi **113** (12%), Mkoa wa Kusini Pemba kesi **121** (13%) na kesi kidogo zimeripotiwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba **58** (6%) ukilinganisha na idadi ya kesi hizo katika Mikoa/Sehemu nyengine.

*Jaduweli Nam 7: Idadi ya kesi kulingana na Sehemu iliyoripoti kesi hizo mwaka 2019-2020*

| SEHEMU | IDADI YA KESI | | JUMLA YA WATUHUMIWA | | IDADI YA WATUHUMIWA | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | 2019 | 2020 | W'ME | W'KE |
| ADU | 114 | 87 | 118 | 95 | 115 | 3 |
| MJINI MAGHARIBI | 156 | 135 | 163 | 142 | 159 | 4 |
| KASKAZINI UNGUJA | 67 | 46 | 71 | 48 | 69 | 2 |
| KUSINI UNGUJA | 83 | 90 | 90 | 90 | 87 | 3 |
| KASKAZINI PEMBA | 25 | 33 | 26 | 33 | 26 | 0 |
| KUSINI PEMBA | 58 | 63 | 58 | 66 | 58 | 0 |
| **JUMLA** | **503** | **454** | **526** | **474** | **514** | **12** |

***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***

Idadi ya kesi za Dawa za Kulevya katika mwaka 2020 imepungua kwa asilimia 9.7 ukilingana na mwaka 2019 (*kutoka kesi 503 mwaka 2019 hadi kesi 454 mwaka 2020*), kutokana na kupungua idadi ya kesi hizo karibu katika kila eneo lililoripoti kesi kwa mwaka 2020. Aidha, kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi katika Mkoa wa Mjini Magharibi kunakoambatana na idadi kubwa na mchanganyiko wa wakaazi kunakadiriwa kupelekea kuongezeka kwa shughuli za usambazaji na utumiaji wa Dawa za Kulevya. Hii inaonesha uwepo wa haja ya kuimarisha zaidi mikakati ya mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya hasa katika maeneo yaliyoathirika zaidi.


Kwa mujibu wa taarifa za uchunguzi wa kimaabara kutoka kwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali juu ya vielelezo vya Dawa za Kulevya vilivyokamatwa na kuchuguzwa ni kwamba kesi zote zilizoripotiwa mwaka 2019-2020 zilihusisha Dawa za Kulevya aina ya Bangi, Heroini, Mirungi, Kokeni na Valiam.

### 3.1.3 Mchanganuo wa Viwango vya dawa kimaeneo ya ukamataji

Vielelezo vifuatavyo vinaonesha mchanganuo wa viwango vya dawa mbali mbali vilivyokamatwa katika maeneo mbali mbali kulingana na Mamlaka za Jeshi la Polisi zilizoripoti viwango hivyo.

**Heroini**


*Kielelezo namba.5 kiwango cha heroin kilichokamatwa 2019-2020*




***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***

**Bangi**


*Kielelezo namba.6 kiwango cha Bangi kilichokamatwa 2019-2020*




***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***

## Mirungi


Kielelezo namba.7 kiwango cha mirungi kilichokamatwa 2019-2020




*Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021*

## Valiam


*Kielelezo namba.8 kiwango cha valiam kilichokamatwa 2019-2020*




*Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021*

## Kokeni

*Kielelezo namba.9 kiwango cha Kokeni kilichokamatwa 2019-2020*




*Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021*

## 3.2 MALI ZILIZOHUSIKA NA UHALIFU WA DAWA ZA KULEVYA

Sheria ya Dawa za Kulevya kifungu cha 43 (1) - (4) kinaeleza kuwa kifaa, mali, chombo ama bidhaa zilizotumika kufichia dawa za kulevya na chumo linalotokana na mauzo ya dawa za kulevya au kitu chengine chochote kinachohusiana na kosa basi kitaifishwe. Katika utekelezaji wa kifungu hicho cha sheria Serikali imeendelea kuzuia na kuzihusisha katika kesi mali mbalimbali zinazohusiana na uhalifu wa Dawa za kulevya hapa Zanzibar. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2020 jumla ya vyombo **15** vya usafiri vilivyohusika na uhalifu huo vimeshikiliwa na kesi zake zinaendelea Mahkamani. Aina ya vyombo hivyo ni kama inavyoonekana katika jaduweli lifuatalo:

*Jaduweli Nam. 8: Idadi ya vyombo vilivyohusishwa na uhalifu wa dawa za kulevya mwaka 2019-2020*

| AINA YA CHOMBO | IDADI | | HATUA YA KESI |
|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | |
| **Honda Click** | 3 | - | Zote zinaendelea mahkamani |
| **Honda Pikipiki** | 2 | - | Kesi 1 bado inaendelea Mahkamani, na kesi 1 imeondolewa Mahkamani |
| **Gari IST** | 4 | 1 | Kesi zote zinaendelea Mahkamani |
| **Gari Rectus** | 1 | - | Inaendelea Mahkamani |
| **Gari Townhiace** | 1 | - | Inaendelea Mahakamani |
| **Gari Porte** | 1 | - | Inaendelea Mahkamani |
| **Gari Rover4** | - | 1 | Inaendelea Mahkamani |
| **Gari ToyotaBB** | - | 1 | Inaendelea Mahakamani |

***Chanzo: Jeshi la Polisi, 2021***

## 3.3 MAFUNZO, MIKUTANO NA VIKAO.

Moja kati ya mikakati ya kupambana na Dawa za Kulevya ambayo imetekelezwa katika kipindi cha 2019 - 2020 ni kufanya mafunzo, vikao na mikutano mbali mbali na wahusika wa mapambano dhidi ya dawa hizo, wakiwemo wasimamizi wa Sheria (Jeshi la Polisi, vyombo vya ulinzi, na mamlaka nyengine zinazohusika na mapambano ya Dawa za kulevya) na viongozi wa madiko.

### 3.2.1 Mikutano ya Wasimamizi wa Sheria

Jumla ya mikutano mitatu (3) ya Wasimamizi wa Sheria juu ya mustakbali mzima wa mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya ilifanyika nchini mwaka 2019 – 2020, iliyojumuisha

wahusika kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Idara ya Usalama wa Taifa, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Kitengo cha Polisi cha Kupambana na Dawa za Kulevya, Jeshi la Polisi na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Mikutano hii ililenga kujitathmini juu ya kesi zilizoripotiwa na majalada yake kufika Mahakamani, kupima maamuzi yaliyotolewa na Mahakama kama yanaendana na kasi ya mapambano pamoja na nadharia nzima ya utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

### 3.2.2 Mafunzo kwa Wahusika wa Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya

Katika kipindi cha miaka miwili (2019 -2020) Serikali iliendesha Mafunzo kwa maofisa wa Polisi upelelezi wa Mikoa ya Pemba yaliyolenga kuboresha mbinu bora za upelelezi ili kuhakikisha kuwa kesi za Dawa za kulevya zinapata hukumu sahihi Mahkamani.

Aidha, katika kipindi hicho Serikali ilifanikiwa kuendesha mafunzo kwa wadau wa madiko katika bandari zisizo rasmi ambapo jumla ya shehia **53** kwa Unguja na **62** kwa Pemba zilipatiwa mafunzo juu ya marekebisho ya sheria ya udhibiti wa Dawa za Kulevya. Katika mafunzo hayo viongozi wa madiko na shehia wametakiwa kuwaelimisha wananchi wao juu ya mabadiliko hayo ili jamii ielewe hatari ya kujihusisha kwa njia moja au nyengine na matumizi na usambazaji wa dawa za kulevya.

### 3.2.3 Vikao vya Tume na vya Kamati ya Kitaalamu

Tume ilifanikiwa kufanya vikao saba (7) vikiwemo vitatu (3) vya Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na vikao vinne (4) vya Kamati ya Kitaalamu ya Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar .Vikao hivi hujadili masuala makuu katika uendeshaji wa Tume.

### 3.2.4 Mikutano ya Uchunguzi na Operesheni

Jumla ya mikutano saba (7) ya operesheni imefanyika ndani ya mwaka 2019 -2020. Mikutano hiyo ilihusisha Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa kwa lengo la kuhakikisha kuwa mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanashushwa katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Shehia. Kamati hizi zimeahidi kuanzisha utaratibu maalumu wa kuyatambua maeneo yalioathirika na biashara pamoja na matumizi ya dawa hizo na kuhakikisha kuwa operesheni maalumu zitalenga maeneo hayo. Pia, mikutano hii ilihusisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Idara za Upelelezi za Mikoa na Wilaya za Unguja na Pemba kutoka Jeshi la Polisi, Kitengo cha Polisi cha Kupambana na Dawa za Kulevya, Idara ya Usalama wa Taifa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA).

# SEHEMU YA NNE

# JUHUDI ZA SERIKALI KATIKA KUPUNGUZA MATUMIZI NA MADHARA YA DAWA ZA KULEVYA

## 4.1 ELIMU JUU YA ATHARI YA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

Katika kipindi cha mwaka 2019 -2020 elimu ya athari ya matumizi ya dawa za kulevya ilitolewa kwa njia ya vipeperushi, kupitia vyombo vya habari pamoja na kuyafikia makundi mbali mbali wakiwemo wanafunzi na walimu wa skuli za Msingi na Sekondari, wanafunzi wa vyuo vikuu pamoja na wafanyakazi wa vikosi vya ulinzi na usalama.

### 4.1.1 Kuyafikia makundi mbalimbali

Jumla ya watu **16,534** Unguja na Pemba walifikiwa katika kutoa elimu ya athari ya Dawa za Kulevya mwaka 2019 - 2020. Idadi hiyo inajumuisha wanafunzi **15,742** na walimu **569** wa skuli za msingi na sekondari Unguja na Pemba, wanafunzi hao wanatoka katika skuli **144** (Unguja **89** na Pemba **55**). Idadi ya wanafunzi wa vyuo waliofikiwa ni **135** na wafanyakazi **88** kutoka vikosi vya ulinzi na usalama.

*Jaduweli Nam.9: Idadi ya waliopatiwa elimu juu ya athari ya matumizi ya Dawa za Kulevya mwaka 2019 - 2020*

| | 2019 - 2020 | | |
|---|---|---|---|
| | **w'me** | **w'ke** | **Jumla** |
| **Wanafunzi wa skuli** | 6274 | 9468 | 15,742 |
| **Walimu** | 333 | 236 | 569 |
| **Wanafunzi wa vyuo vikuu** | 88 | 47 | 135 |
| **Vikosi vya ulinzi** | 62 | 26 | 88 |
| **Jumla Kuu** | | | **16,534** |

***Chanzo: TKKUDK,2021***

### 4.1.2 Kutoa vipeperushi

Kwa upande wa elimu kwa njia ya vipeperushi, jumla ya vipeperushi 7,000 vilichapishwa na kusambazwa kwa watu na katika maeneo mengine mbalimbali. Vipeperushi hivyo vililenga kutoa ujumbe unaoelimisha juu ya athari za matumizi ya Dawa za Kulevya.

### 4.1.3 Kurusha vipindi vya Redio na Televisheni

Aidha, elimu hiyo pia imetolewa kupitia vyombo mbali mbali vya habari nchini, ambapo jumla ya vipindi **33** vilirushwa hewani katika redio na televisheni za ZBC, Mwenge FM, Bomba FM, Hits FM, Coconut FM, Zenji FM, TIFFU TV na Zanzibar Cable TV. Mada kadhaa zilijadiliwa zikiwemo Athari ya matumizi ya Dawa za Kulevya, Sheria ya Dawa za kulevya, elimu ya kinga

ya msingi (primary prevention), huduma za upataji nafuu, watumiaji wa dawa za kulevya na maambukizi ya Covid-19 na tiba za kifamilia.

## 4.2 KINGA YA MSINGI DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA

Kinga ya Msingi ni mpango maalumu wenye lengo la kutoa elimu yenye kusaidia jamii hususan watoto na vijana ili wajiepushe na kuanza kutumia dawa za kulevya au kutokuanza kutumia dawa hizo wakiwa katika umri mdogo. Kwa kipindi cha 2019 - 2020 TKKUDK iliendesha programu ya kinga ya msingi kwa kutoa taaluma ya athari ya dawa za kulevya kwa watoto wa skuli **4** za maandalizi ambazo ni Jang'ombe, Kidutani, Saateni na Magomeni. Katika programu hiyo jumla ya wanafunzi **412** na walimu **9** walipatiwa elimu juu ya athari ya Dawa za Kulevya. Kati ya hao wanafunzi **192** walikuwa wa kiume na **220** walikuwa wa kike na walimu wote walikuwa ni wakike. Mchanganuo wa idadi hiyo unaonekana katika **Jaduweli Nam.6**

*Jaduweli Nam.10: Idadi ya waliopatiwa elimu juu ya athari ya Dawa za Kulevya kupitia program ya kinga ya msingi mwaka 2019-2020*

| SKULI ZA MAANDALIZI | WANAFUNZI | | WALIMU | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | |
| JANG'OMBE | 63 | 55 | 2 | 0 | 120 |
| KIDUTANI | 71 | 64 | 2 | 0 | 137 |
| SAATENI | 39 | 33 | 2 | 0 | 74 |
| MAGOMENI | 47 | 40 | 3 | 0 | 90 |
| **JUMLA KUU** | **220** | **192** | **9** | **0** | **421** |

***Chanzo: TKKUDK,2021***

## 4.3 KUZIWEZESHA PROGRAMU ZA UPATAJI NAFUU.

Serikali imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuziwezesha programu za upataji nafuu zinazoendeshwa na taasisi mbali mbali zikiwemo taasisi binafsi na za kiserikali. Programu hizo ni Nyumba za upataji nafuu (Sober House), mikutano ya tiba za kifamilia (Family Therapy) na kuwajengea uwezo watumiaji baada ya kupata nafuu.

### 4.3.1 Kusaidia nyumba za upataji nafuu (Sober Houses)

Tume imezipatia ruzuku nyumba **8** za upataji nafuu (Sober Houses) Unguja na Pemba katika kipindi cha miaka miwili 2019 - 2020 kwa lengo la kusaidia uendeshaji wa nyumba hizo ili kuiokoa jamii na janga la matumizi ya Dawa za Kulevya. Nyumba hizo ni Trent, Detroit, Zanzibar Youth Forum, Free At Last,Tawabina na Nyarugusu kwa Unguja, na kwa upande wa Pemba ni Mkoroshoni(Chake) na UMATI (Wete).

Idadi ya watumiaji waliopokelewa katika nyumba hizo kwa kipindi hicho imefikia **750** kama inavyoonekana katika Jaduweli namba 7.

*Jaduweli Nam.11 Idadi ya watu waliojiunga na huduma ya upataji nafuu kwa mwaka 2019-2020*

| MIAKA | 2019 | | | 2020 | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | |
| 18-25 | 50 | 0 | 50 | 53 | 0 | 53 | **103** |
| 26-35 | 214 | 0 | 214 | 148 | 0 | 148 | **362** |
| 36-45 | 100 | 0 | 100 | 95 | 0 | 95 | **195** |
| 46+ | 37 | 0 | 37 | 53 | 0 | 53 | **90** |
| | | | | | | | **750** |

***Chanzo: TKKUDK, 2021***

### 4.3.2 Mikutano ya Tiba ya Kifamilia

Katika kuziwezesha programu za upataji nafuu, Tume ilifanya mikutano saba (**7**) ya Tiba ya kifamilia (Family Therapy), mikutano (**4**) Unguja na (**3**) Pemba. Mikutano hiyo ilizishirikisha jumla ya familia 240 za wazazi/walezi wenye vijana wanaotumia Dawa za Kulevya na waliopata nafuu. Familia 92 zilitoka katika maeneo mbalimbali ya kisiwa cha Pemba ikiwemo Wete, Kangagani, Wambaa, Chake chake, Tumbe, Chasasa, Selemu, Utaani, Konde, Wingwi, Mtemani, Kipangani, Ole na kwengineko. Familia **148** zilizoshiriki zilitoka katika maeneo ya Unguja ikiwemo Kikwajuni, Kijitoupele, Fukuchani, Kitumba, Kinuni, Dunga, Jang'ombe, Fuoni, Mangapwani, Vikokotoni, Kihinani, Muembetanga, Shangani, Mwanyanya, Mahonda, Mkwajuni na kwengineko. Mikutano hiyo inalenga kuzungumza na wazazi/walezi wa watoto hao ili kuwapa nafasi ya kueleza changamoto zinazowakabili katika kuwasaidia watoto wao, kuwasaidia wazazi/walezi hao kupunguza msongo wa mawazo na kuwafariji ili kupata nguvu za kuwasaidia watoto wao kupata huduma ya upataji nafuu.

### 4.3.3 Kuwajengea uwezo watumiaji baada ya kupata nafuu

Katika kuwajengea uwezo vijana waliopata nafuu, Tume imemdhamini kijana mmoja (1) alieamua kuachana na matumizi ya dawa za kulevya kwenda kusoma masomo ya Utalii (Tourism information) ngazi ya cheti, katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

### 4.3.4 Kupunguza Madhara ya kiafya kwa watumiaji wa Dawa za Kulevya

Katika kupunguza madhara ya kiafya kwa watumiaji wa Dawa za kulevya mbalimbali waliwezeshwa kushiriki mikutano ya ngazi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa katika sehemu tofauti zikiwemo Arusha, Austria, Kenya, Afrika Kusini na nyenginezo. Aidha, kuwawezesha Jumuiya ya ZANPUD (Zanzibar Network for People who Used Drugs) kuwa wajumbe katika

*East African Harm Reduction na AfricanPUD*, na kupitia taasisi hiyo Zanzibar imepata nafasi ya uwenyekiti wa *East African Harm Reduction.*

## 4.4 KUENDESHA MIKUTANO YA WADAU

Katika mwaka 2019-2020 ilifanyika mikutano saba (7) ya wadau walioachana na matumizi ya Dawa za Kulevya yenye lengo la kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa nyumba za upataji nafuu. Mikutano hiyo imelenga kuimarisha mikakati ya kupunguza mahitaji ya Dawa za Kulevya na kusaidia upataji nafuu kwa watumiaji, kutathmini mafanikio yaliyofikiwa pamoja na tahadhari na mbinu za kujikinga na Maambukuzi ya maradhi ya Covid-19 katika nyumba hizo.

## 4.5 KITUO CHA TIBA NA MAREKEBISHO YA TABIA - KIDIMNI

Katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2010 -2015 Ibara ya 155(b) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imefanya jitihada katika utekelezaji wake wa majukumu ya kisheria kwa kuanzisha ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa vijana walioathirika na matumizi ya Dawa za Kulevya ili kuwatibu vijana hao, kituo hicho kinategemea kuanza kutoa huduma katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kituo hicho kinalenga kuhudumia waathirika wa Dawa za Kulevya waliopo Zanzibar, Tanzania bara pamoja na raia wengine kutoka nchi mbalimbali duniani. Kituo kitatoa huduma za matibabu, marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa Dawa za Kulevya pamoja na mafunzo mbalimbali ya ujasiri amali miundo mbinu yake itakapokamilika.

# SEHEMU YA TANO

# USHIRIKIANO WA NDANI YA NCHI NA WA KIMATAIFA

## 5.1 USHIRIKIANO NA TAASISI ZA NDANI YA NCHI

Tume imekuwa ikitekeleza majukumu yake kisheria kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za ndani ya nchi ambazo kwa njia moja au nyengine zinajukumu la kupambana na Dawa za Kulevya au kutoa huduma za Tiba kwa wale ambao wameathirika kutokana na matumizi ya Dawa za Kulevya.

Baadhi ya Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo Tume inashirikiana nazo ni Jeshi la Polisi, Idara ya Usalama wa Taifa, Idara ya Uhamiaji, Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania, "Financial Intelligence Unit" (FIU) na Chuo kikuu cha Sayansi na Afya Muhimbili.

Aidha,Tume imekuwa na mashirikiano ya karibu na Taasisi za SMZ zikiwemo: Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Shirika la Bandari Zanzibar, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Tume ya UKIMWI, Kitengo Shirikishi cha UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibar na nyenginezo.

Vile vile,Tume imeshirikiana na taasisi zisizokuwa za Serikali zikiwemo MIMI na WEWE Foundation, "Zanzibar Youth Education Development Support Association"(ZAYEDESA), Jumuiya ya wanaotumia Dawa Saidizi (MAT), Chama cha Uzazi na Malezi bora Tanzania (UMATI), Jumuiya ya Kuelimisha Athari za dawa ya Kulevya Ukimwi na Mimba katika Umri Mdogo (JUKAMKUM), Jumuiya ya Upataji Nafuu Zanzibar (RCZ), Jumuiya ya Vijana Zanzibar (ZYF), Free at Last, Taasisi za dini, Jumuiya ya Mtandao wa Waliotumia Dawa za Kulevya Zanzibar (ZANPUD), Drug Free Zanzibar (DFZ), TAWWABINA, Corner Stone, Chama cha Waandishi wa Habari Zanzibar, Jumuiya ya Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi Zanzibar (ZAPHA+) na nyenginezo.

## 5.2 USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

Katika kudhibiti usambazaji, usafirishaji na matumizi ya Dawa za Kulevya Zanzibar, Serikali imeshirikiana na taasisi mbalimbali za Kikanda na za Kimataifa zinazoshiriki mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya katika kuandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali itakayofanikisha udhibiti huo.

### 5.2.1 SHIRIKA LA KIMATAIFA LA KUZUIA UHALIFU NA DAWA ZA KULEVYA (UNODC)

- Watendaji sita wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) wanatarajia kushiriki mafunzo ya kudandia meli, upekuzi na uzuiaji wa meli (Training in Vessel Boarding, Search and Seizure "VBSS") yatakayofanyika katika Chuo cha Kikosi cha Ulinzi wa Bahari huko *Mahe* nchini *Sychelles* kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC).

- Serikali kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za kulevya kwa kushirikiana na UNODC imetoa mafunzo kwa washirika wa mapambano ya Dawa za Kulevya katika bandari wakiwemo Polisi, Shirika la Bandari, KMKM, Idara ya Usalama wa Taifa na Mamlaka ya mapato Tanzania kuhusiana na uendeshaji wa programu ya udhibiti na ukaguzi wa makontena. Programu hiyo ina lengo la kukagua makontena yote yatakayoingia na kutoka Bandarini Zanzibar ili kuyatambua makontena yatakayokuwa na bidhaa haramu zikiwemo Dawa za Kulevya.

- Serikali kwa kushirikiana na UNODC imeendelea kuendesha programu ya kuimarisha familia (strong family) inayohusu kinga ya msingi dhidi ya Dawa za Kulevya (Primary prevention), pamoja na kupanga mikakati ya kuendeleza pragramu hii kwa siku zijazo. Programu hii ni kwa ajili ya wazee wa watoto ambao hawajaingia katika matumizi ya Dawa za Kulevya ambapo utekelezaji wake umeanza kwa vijiji vinne vya Wilaya ya Kati vilivyochaguliwa ambavyo ni Uroa, Pongwe, Kiboje na Dunga.

### 5.2.2 DRUG ENFORCEMENT ADMINISTRATION (DEA)

- Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imefanya mazungumzo na taasisi inayoshughulikia mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya ya Marekani (Drug Enforcement Administration) kujadili jinsi ya kushirikiana katika mapambano ya Dawa za Kulevya. Kupitia mazungumzo hayo Serikali imeanza kutoa mafunzo ya mbinu za upelelezi kwa Askari wa Upelelezi wa Mikoa mitatu ya Unguja yaliyofanyika katika Chuo cha Polisi Zanzibar.

- Aidha, Maafisa wawili wa Kitengo cha Polisi cha Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar wameshiriki mafunzo ya udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini Botswana (ILEA) kwa udhamini wa taasisi hiyo hiyo (Drug Enforcement Administration).

### 5.2.3 UNITED KINGDOM (UKaids) & UK BORDER FORCE

- Kupitia mazungumzo yaliyofanyika baina ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Shirika la "*UKaids"* juu ya kushirikiana katika mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya, shirika hilo limekubali kuisaidia Zanzibar na limetenga Shilingi Bilioni Nne kwa ajili ya kupambana na uhalifu uliopangwa. Taarifa juu ya mradi huo imewasilishwa Tume na hatimae imefikishwa katika Baraza la Mapinduzi.
- Aidha kwa upande wa UK Border Force, shirika hili linaendelea kushirikiana kwa karibu sana na jeshi la polisi katika kudhibiti usafirishaji wa Dawa za Kulevya kupitia Uwanja wa ndege wa Zanzibar, shirika hilo limetoa mchango mkubwa kwa kuwapatia mafunzo askari hao pamoja na vifaa vya kisasa kwa ajili ya ukaguzi wa abiria na mizigo katika uwanja huo.

### 5.2.4 US DEPARTMENT OF DEFENCE

- Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imekutana na ujumbe wa Watu wa Marekani kutoka Idara ya Ulinzi (US Department of Defence) na Idara Maalum inayoshughulika na Dawa za Kulevya Kimataifa (US Department of State – Bureau of International Narcotics and Law Affairs) kwa lengo la kushirikiana katika udhibiti wa Dawa za Kulevya katika maeneo ya bahari. Ujumbe huo umeahidi kuisaidia Zanzibar katika kutatua changamoto zilizopo katika kukabiliana na usafirishaji wa Dawa za Kulevya hasa kwa maeneo ya bahari na wameonesha nia ya kufanya kazi pamoja na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) baada ya kukamilika kwa mazungumzo baina ya taasisi hizo.

# SEHEMU YA SITA

# MAFANIKIO, CHANGAMOTO, HATUA ZA BAADAE NA HITIMISHO

## 6.1 MAFANIKIO

Serikali kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya katika jitihada za kupambana na Dawa za kulevya ndani ya mwaka 2019 -2020 imepata mafanikio mbalimbali miongoni mwa hayo ni kama ifuatayo.

**a.** Kuifanyia marekebisho makubwa *Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nam.9 ya mwaka 2009. Marekebisho hayo yakiwemo*
   - Kushughulika na mali zilizohusishwa na zilizochumwa kutokana uhalifu wa dawa za kulevya.
   - Kuongeza viwango vya adhabu.
   - Katazo la kemikali bashirifu.

**b.** Kupunguza usambazaji wa Dawa za Kulevya kwa kukamata viwango vikubwa vya dawa za kulevya kabla ya kuwafikia watumiaji. Hii imetokana na kuimarika kwa mashirikiano ya Kitaifa , kikanda ma kimataifa ambayo yamepelekea kukua kwa mawasiliano.

**c.** Serikali kupitia Tume imefanikiwa kutoa mafunzo ya *Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya* na marekebisho yake katika ngazi zote kuanzia Taifa, Mikoa, Wilaya, Shehia hadi ngazi ya Familia.

**d.** Mafunzo ya upelelezi yanayotolewa kwa jeshi la polisi na wasimamizi wengine wa sheria yameongeza ufanisi katika ukamataji na uendeshaji wa kesi za dawa za kulevya jambo linalopelekea kupungua kwa ufungaji wa kesi vituoni na Mahkamani na kuongezeka kwa idadi ya kesi zinazopata hatia.

**e.** Kuanzisha programu ya kinga ya msingi dhidi ya matumizi ya Dawa za Kulevya kwa watoto waliopo katika ngazi ya elimu ya maandalizi.

**f.** Kusambaratisha na kuvunja maduka makubwa ambayo yalitumika kwa uhalifu huu wa Dawa za Kulevya.

**g.** Kuendeleza hatua za ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia Kidimni kwa; maumbo ya ghorofa ya kwanza na ya pili ya jengo kuu, kuezeka pamoja na kukamilisha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuendeshea kituo hicho.

**h.** Kushiriki kikamilifu katika mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ambayo imesaidia kukuza mashirikiano na mawasiliano na taasisi mbalimbali zenye kupambana za Dawa za Kulevya duniani.

**i.** Kupunguza unyanyapaa kwa walioacha kutumia Dawa za Kulevya hivyo kuwasaidia watumiaji hao kupata huduma muhimu.

**j.** Kuongezeka kwa vijana walioachana na Matumizi ya Dawa za Kulevya Zanzibar.

## 6.2 CHANGAMOTO

Katika utekelezaji wa shughuli zake ilizojipangia Tume ilikabiliana na changamoto mbalimbali zikiwemo:

a. Maumbile ya nchi yetu yanayoruhusu uwepo wa bandari nyingi zisizo rasmi(zaidi ya 271 Unguja na Pemba) ambapo ikizingatiwa kuwa kuna uhafifu wa vifaa vya ulinzi na utambuzi vya kutosheleza maeneo yote ya Visiwa.
b. Uwepo wa Visiwa vya Zanzibar katika mwambao wa Afrika Mashariki pia ni changamoto kwani Vyombo vya Kimataifa vimeutambua ukanda huu kuwa ni njia inayotumika kupitishia Dawa za Kulevya kutoka Nchi uzalishaji heroini (Afghanistani) na kuelekea Asia, Marekani na Ulaya.
c. Ukosefu wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya udhibiti wa usafirishaji wa Dawa za Kulevya katika mipaka yetu.
d. Kuwepo kwa viashiria vya rushwa kunakotokana na kutokuwepo uadilifu kwa baadhi ya wasimamizi wa Sheria katika utekelezaji wa Sheria na harakati za udhibiti wa Dawa za Kulevya, kwa mfano kuwepo ucheleweshwaji wa kesi na maamuzi ya kesi yaliyo kinyume na Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya.
e. Wasimamizi wa sheria wanakosa taaluma ya kutosha katika masuala ya upelelezi wa mali za wahalifu wa Dawa za Kulevya.
f. Taasisi iliyopo sasa haina uwezo wa kisheria wa kuchunguza, kukamata, kupeleleza na kupeleka kesi mahkamani.

## 6.3 HATUA ZA BAADAE

Serikali Kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imepanga kutekeleza kazi zifuatazo katika harakati za kufanikisha mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya.

i. Kufanya marekebisho ya sheria itakayoanzisha taasisi yenye Mamlaka kisheria ya kuchunguza, kukamata, kupeleleza na kupeleka kesi mahkamani.

ii. Kuendeleza kazi za udhibiti wa Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya katika mipaka na maeneo hatarishi kwa kutumia vifaa na teknolojia za kisasa.

iii. Kuimarisha na kuendeleza kituo cha pamoja cha uendeshaji wa kesi za Dawa za Kulevya kwa kukamilisha muongozo wa uendeshaji wa kituo hicho (One Stop Centre).
iv. Kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa jamii juu ya athari za matumizi ya Dawa za Kulevya na kuimarisha kinga ya msingi dhidi ya matumizi ya Dawa za Kulevya.
v. Kuendelea kuziwezesha Programu za Upataji Nafuu.
vi. Kuendesha Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kilichopo Kidimni.
vii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kuimarisha utendaji wa kazi kuendana sambamba na kasi ya mapambano ya dhidi ya Dawa za Kulevya.
viii. Kuimarisha mahusiano na taasisi nyengine za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika udhibiti wa Dawa za Kulevya.
ix. Serikali ianzishe Mamlaka ya kupambana na dawa za kulevya nchini itakayokuwa na uwezo wa kuchunguza, kukamata, kupeleleza, kuzuia mali, kuzuia akaunti na kufungua mashtaka mahkamani.
x. Kujenga kituo cha Tiba na Marekebisho ya tabia kwa waathirika wa Dawa za Kulevya za Kulevya Pemba kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 196 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020- 2025.

**6.4 HITIMISHO**

Pamoja na kuona changamoto mbalimbali zinazokabili harakati za kupambana na usambazaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya na hatua zilizochukuliwa kutatua changamoto hizo, bado jitihada zaidi za kila mdau zinahitajika ili kuinusuru jamii na taifa kwa ujumla kutokana na athari zinazotokana na janga la dawa za kulevya na hatimaye kuwa na taifa lenye nguvu kazi itakayoleta tija katika kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla kwa maslahi mapana ya Taifa letu.